## 4. Wajumbe/ Washauri (Assessors) wa Baraza

Mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ni mfumo shirikishi kwasababu unawashirikisha wananchi katika kutatua migogoro yao, kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Mahakama Kuu-Idara ya Ardhi. Wananchi wanashiriki kutokana na baadhi yao kuteuliwa kuwa wajumbe au washauri (Assessors) wa Baraza. Kwamujibu wa Sheria Na.5 ya mwaka 1999, Baraza la Ardhi la Kijiji lina wajumbe saba (7) na lazima watatu (3) kati yao wawe ni wanawake. Wajumbe hao wanateuliwa na Halmashauri ya Kijiji na majina yao yanafikishwa kwenye Mkutano mkuu wa Kijiji ili yathibitishwe kabla ya kuanza kazi.

Kwa mujibu wa Sheria Na.7 ya mwaka 1985 (The Ward Tribunals Act, 1985) wajumbe wa Baraza la Kata wanatakiwa wawe kati ya wanne (4) na wanane (8) na kati yao watatu (3) lazima wawe wanawake.

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, kwa mujibu wa Sheria Na.2 ya mwaka 2002 (The Land Disputes Courts Act, 2003) lina wajumbe wasiozidi saba (7) na watatu kati yao lazima wawe wanawake. Na wajumbe hawa huteuliwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutokana na mapendekezo ya Mkuu wa Mkoa na lazima wawe wakazi katika eneo la Wilaya husika.

## 5. Sifa za Mjumbe

(a)Awe mtu mwenye heshima, mtu mwenye msimamo na ufahamu wa Sheria za Ardhi za eneo husika

(b) Awe raia wa Tanzania na mkazi wa Kijiji, kata au wilaya husika.

c) Umri wake uwe miaka 18 na kuendelea kwa Baraza la Ardhi la Kijiji, na Baraza la Kata ni miaka 21 na kuendelea na pia kwa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

(d) Awe na akili timamu na asiwe na kumbukumbu zozote za makosa ya jinai

(e) Asiwe mbunge au Hakimu katika Wilaya husika, Diwani au mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya, Kata au Kijiji. Kwa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kiwango cha chini cha elimu ni kidato cha nne (4).

## 6. Uwakilishi

Mawakili hawaruhusiwi kuwawakilisha wananchi katika Baraza la Kata isipokuwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Hata hivyo, kama mtu hawezi kufika mbele ya Baraza la Kata kutokana
na sababu za msingi, Baraza linaweza kumruhusu ndugu Wa karibu kumwakilisha mtu huyo.

## 7. Utekelezaji wa maamuzi ya Baraza

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya hutekeleza hukumu zake lenyewe kwakutumia madalali wake (Tribunal Brokers). Vilevile Baraza hili linasimamia utekelezaji wa hukumu za Baraza la kata ambazo zilikuwa zimeshatolewa kabla ya kufanyiwa marekebisho kwa Sheria Na.2 ya mwaka 2002 yaliyoletwa na kifungu Na. 45 cha Marekebisho ya Sheria Na.3 ya mwaka 2021 (The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, Act No. 3 of 2021) kilichoyaondolea nguvu ya kimahakama Mabaraza ya Kata na kuyataka yafanye usuluhishi tu.

*Mawasiliano ya Wizara*
*Address: S.L.P. 2908, Dodoma.*
*Barua Pepe: ps@lands.go.tz*
*Simu: +255 26 296 3313 / +255 26 296 3314*
*Nukushi: +255 26 296 3316*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**



# MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

# MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI NA NYUMBA

## 1. Utangulizi

Kipeperushi hiki sio tafsiri ya Sheria, bali ni moja ya njia zilizobuniwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kufikisha ujumbe wa kisheria kwa wananchi juu ya Sheria ya Ardhi zinazotoa miongozo na kuanzisha vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Vyombo hivyo ambavyo ni Mahakama kwa mujibu wa Sheria hizi ni:-

i. Baraza la Ardhi la Kijiji (The village Land Council).

ii. Baraza la Kata (The Ward Tribunal).

iii. Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya (The District Land and Housing Tribunal)

iv. Mahakama kuu (The High Court).

v. Mahakama ya Rufaa ya Tanzania (The Court of Appeal of Tanzania).

Mfumo wa utatuzi wa migogoro unaanzia katika ngazi ya Kijiji na unachukua muda mfupi na hutumia taratibu rahisi na shirikishi zisizokuwa na gharama kubwa kwa Watanzania.

## 2. Sheria Na. 2 ya mwaka 2002 (The Land Disputes Courts Act, 2002)

Sheria hii inabainisha kuwa, Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi hazina mamlaka ya kutatua migogoro inayohusisha ardhi na nyumba

Sheria hii imeweka wazi vyombo vilivyoundwa kisheria katika kutatua migogoro ya ardhi na nyumba, vyombo hivyo ni:

(i) Baraza la Ardhi la Kijiji

Baraza la Ardhi la Kijiji lina mamlaka ya usuluhishi na endapo wahusika hawaridhiki na uamuzi wake, wanaruhusiwa kupeleka masuala yao kwenye Baraza la Kata

(ii) Baraza la Kata

Baraza hili linaundwa chini ya Sheria Na.7 ya mwaka 1985 (The Ward Tribunals Act, 1985).

Baraza hili Pamoja na majukumu yake chini ya Sheria No.2 ya mwaka 2002 na marekebisho yake ya mwaka 2021, limeondolewa majukumu yake ya kimahakama ya kusikiliza na kuamua migogoro ya ardhi badala yake limepewa nguvu ya kufanya usuluhishi tu kwenye eneo lake

(iii) Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

Kwamujibu wa kifungu Na. 22 cha Sheria Na 2 ya mwaka 2002, kinampa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya Kuunda Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika Wilaya, Mkoa au Kanda kutegemeana na wingi wa migogoro ya ardhi na nyumba kwenye eneo hilo.

## 3. Kazi za Baraza

Baraza la Ardhi la Kijiji linasuluhisha au linasaidia wananchi wenye migogoro ya ardhi katika Kijiji kufikia muafaka.

• Baraza la Ardhi la Kijiji huitisha kikao baada ya pande zinazohusika kukubali huduma ya upatanishi ya Baraza hilo. Hata hivyo, wananchi hawalazimiki kutumia huduma ya Baraza la Ardhi la Kijiji, na hata kama watatumia huduma hiyo, wanaweza pia kukataa maamuzi yake.

Kwasababu hiyo, wananchi wanaweza kupeleka masuala yao moja kwa moja kwenye Baraza la Kata.

• Kazi ya Baraza la kata ni kufanya usuluhishi tu, na sio kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya migogoro ya ardhi kwenye eneo lake.

• Hakuna uwakilishi wa Mawakili kwenye Baraza la Kata.

• Kazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ni kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya migogoro yote ya ardhi na nyumba ndani ya eneo lake la kimamlaka.

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya linapokea migogoro yote ambayo thamani ya nyumba, ardhi au kinachodaiwa hakizidi Milioni mia Mbili (200,000,000) kwa vitu vinavyohamishika na Milioni mia tatu (300,000,000) kwa vitu visivyohamishika.